# Maswali na Majibu

**Fursa ya fidia kwa makundi ya majadiliano ya lugha anuwai yanayomilikiwa na jamii**

*Yalichapishwa kwenye tovuti ya Philadelphia City Fund: [https://philacityfund.org/polyglot-philadelphia/](https://philacityfund.org/polyglot-philadelphia/)*

Philadelphia City Fund, Ofisi ya Wahamiaji, Ofisi ya Ubunifu na Teknolojia hivi majuzi zilitangaza fursa kwa makundi ya majadiliano yanayofidiwa kutathmini mahitaji ya mawasiliano ya wanajamii wa lugha anuwai katika Jiji la Philadelphia na kuchangia kwenye dhamira ya Programu ya Ufikiaji wa Lugha Philly ya "Kuhakikisha kuwa watu wote wanaweza kufikia huduma za Jiji kwa lugha yao." Fursa hii imewezeshwa kutokana na ruzuku ya Operation Transformation Fund ili kuimarisha tafsiri kwenye Phila.gov.

**Maswali yaliyopokelewa kuhusu fursa, pamoja na majibu ya Ofisi ya Wahamiaji, yamejumuishwa hapa chini. Waraka huu utaendelea kusasishwa maswali yanapopokelewa na tafsiri zitachapishwa pindi zinapokuwa tayari.**

1. **Je, makataa ya fursa hii ni ya lini? Je, ni tarehe 10 Apriliau tarehe 20 Aprili?**

   Makataa ya fursa hii ni Alhamisi, tarehe 20 Aprili, 2023.

   Kwa ufafanuzi zaidi, tumeweka makataa tofauti ya Jumatatu, tarehe 10 Aprili, 2023 ya kukubali maswali ili kuweza kutoa majibu yaliyotafsiriwa kabla ya dirisha la utekelezaji kufungwa.

2. **Je, makundi au watu binafsi wasioshirikishwa wanaweza kuwasilisha ombi?**

   Hapana, miongozo inabainisha kuwa mashirika yanahitaji kuweza kutoa fomu ya W-9. Njia nyingine ni kuomba ufadhili wa fedha, au kutuma ombi kupitia shirika bia.

3. **Sisi [kundi] tumekuwa tukishughulikia taratibu za kuwezesha ombi letu na tunakumbana na changamoto za taratibu. Hatujaweza kupata mfadhili wa fedha kutoka shirika lisilo la faida. Tuliwazia kuanzisha LLC yetu lakini hilo pia litachukua muda mrefu na taratibu ambazo hatuwezi kushughulikia kabla ya makataa. Tunajaribu kufikiria hatua bora ya kuchukua kwa kuzingatia hali. Tungependa kutimiza fursa lakini tumezuiwa na changamoto hizo.**

   Miongozo inabainisha kwamba ni mashirika pekee yanayoweza kutuma ombi -- hii si fursa ya watu binafsi. Unaweza kutuma ombi kupitia mfadhili wa fedha au shirika bia, ambalo linaweza kuwa shirika linaloweza kutoa fomu ya W-9 (fikiria mashirika ya kidini, biashara ndogondogo, LLC, mashirika yasiyo ya faida, n.k.) Siku zijazo, tunaweza kufikiria njia mbadala za kufidia makundi yasiyoshirikishwa, lakini tumeshindwa kutoa nafasi kwa ajili ya fursa hii ya fidia kwa kuwa tutahitaji kubadilisha miongozo yetu.

4. **Je, mashirika yanaweza kuwa na makundi anuwai ya majadiliano katika lugha moja? Kwa mfano, makundi 2 tofauti ya Kifaransa na Kiarabu?**

   Mashirika yanaweza kufanya zaidi ya lugha moja ikiwa hilo limo ndani ya uwezo wayo. Kiasi cha fidia kitakuwa $5,000 kwa kila shirika. Kutoka kwenye miongozo:

*Lazima [anayetuma ombi] aweze kuajiri na kuwasiliana na wasemaji wa* ***angalau*** *moja ya makundi ya lugha zifuatazo:*

a. *Kiarabu*
b. *Kichina (ikiwa ni pamoja na Kimandarini, Kikantoni, au lahaja za wachache)*
c. *Kifaransa*
d. *Kikrioli cha Haiti*
e. *Kireno*
f. *Kirusi*
g. *Kihispania*
h. *Kswahili*
i. *Kivietnamu*
j. *Lugha tofauti (isipokuwa Kiingereza)*

5. **Je, kuna fomu ya kuripoti bajeti itakayohitajika kutolewa na mashirika kama sehemu ya kuripoti huku?**

   Ofisi ya Wahamiaji haihitaji kuwasilisha fomu ya bajeti kwa ajili ya kuripoti. Kutokana na miongozo, nyaraka za mradi ambazo lazima ziwasilishwe kwenye Ofisi ya Wahamiaji mwishoni mwa mradi, ni pamoja na:

   a. Fomu za mahudhurio zilizo na sehemu zifuatazo
      i. Jina au lakabu za mshiriki
      ii. Lugha
      iii. Nchi ya kuzaliwa
      iv. Msimbo wa eneo
      v. Anwani ya barua pepe (si lazima)
   b. Ikiwa unarekodi au unapiga picha, kusanya fomu za idhini zilizotiwa sahihi kutoka kwa washiriki
   c. Maelezo ya kundi la majadiliano na chunguzi muhimu
   d. Faharasa iliyo na misamiati muhimu katika lugha lengwa na Kiingereza, yenye ufafanuzi mfupi
   e. Mradi wa sanaa unaowasilisha matokeo ya shirika kwa umma kwa jumla. Tokeo hili liko wazi wa ubunifu wa shirika lililokusanya maoni na huhimiza ubunifu katika matoke ya mradi.

6. **Je, sehemu ya 5 K inaweza kutumika kuwalipa washiriki?**

   $5K ni fursa ya fidia ambayo kila shirika linaweza kutumia linavyopendelea, huku likufuata matokeo ya mradi na kuhakikisha idadi ya chini zaidi ya washiriki kumi. Kutoka kwenye miongozo:

   a. Fidia za $5,000 kila moja zitapewa hadi mashirika 10. Kila shirika litatarajiwa kufanya angalau kundi moja (1) la majadiliano lenye idadi ya chini ya washiriki kumi (10) wanaozungumza na kusoma kwa lugha ambayo ni mbali na Kiingereza. Makundi ya majadiliano yatatambua maudhui yanayofikiwa mara kwa mara kwenye tovuti ya phila.gov na kushiriki matokeo yoyote kuhusu taarifa zinazosemekana si bayana au zimetafsiriwa vibaya.

7. **Kutoka S#9 katika fomu ya ombi, unaweza kubainisha ikiwa shirika lililo na mfadhili wa fedha linastahiki kutuma ombi la fedha hizi? Ikiwa ndivyo, unaweza kutoa nyaraka zozote zinazotakikana ambazo tunahitaji kutoa?**

Ndiyo, mashirika yanaweza kutuma ombi kupitia mfadhili wa fedha. Philadelphia City Fund haihitaji nyaraka zozote za ziada, lakini ombi linapaswa kubainisha mfadhili wa fedha na kwamba shirika au kundi linatuma ombi kupitia mfadhili wa fedha. Mfadhili wa fedha atatoa nyaraka zinazohitajika ambazo zimeelezwa katika miongozo ya ustahiki.

a. Lazima aweze kutoa fomu ya W-9, ankara na Fomu ya ACH ya shirika ili kupokea malipo.
b. Shirika [au mfadhili wa fedha] lazima atoe huduma katika jimbo la Philadelphia kama shirika lililoshirikishwa. Kwa mfano: Mashirika yasiyo ya faida, LLC na biashara zinastahiki.

8. **Kutoka S#13/S#15 katika fomu ya ombi, je, wawezeshaji wafanyakazi na washiriki wanahitaji kuwa wakazi wa jimbo la Philadelphia ili kustahiki kushiriki katika programu hii?**

Miongozo inabainisha kwamba lazima shirika liweze kupanga angalau kundi moja (1) la majadiliano ana kwa ana katika jimbo la Philadelphia na kuwa makundi ya majadiliano yatatambua maudhui yanayofikiwa mara kwa mara zaidi kwenye tovuti ya phila.gov ili kushiriki matokeo kuhusu taarifa zinazosemekana si bayana au zimetafsiriwa vibaya. Kwa hivyo, shirika linahitaji kuhakikisha kwamba matakwa ya chini zaidi yamefidiwa na chochote zaidi ya hapo kitategemea uwezo wa shirika.

Hatukutambua matakwa ya makazi kwa mwezeshaji na tunamhimiza yeyote ambaye angependa kutoa maoni kushiriki, lakini kufahamu kwamba pendekezo lako linapaswa kueleza sababu na jinsi jamii lengwa ingependa kutoa maoni kuhusu Phila.gov na athari kwenye Programu ya Ufikiaji wa Lugha Philly (angalia S#15 na S#18).

9. **Kutoka Q#16 katika fomu ya ombi, je, kuna sifa yoyote ya ustahiki inayotarajiwa kwa wawezeshaji wa lugha mbili? Na je, kuhusu miongozo yoyote ya kuhakikisha uanuwai miongoni mwa washiriki kutoka kundi la lugha moja? Tabaka, jinsia, utaifa, hali ya jamii na uchumi (Mfano, elimu)**

Shirika ambalo lingependa kuwasilisha ombi linaweza kutambua sifa za ustahiki za wawezeshaji wake. Ofisi ya Wahamiaji haitatoa matakwa ya chini zaidi kwa sababu hii ni fursa inayomilikiwa na jamii na tunataka kuondoa vikwazo na kujifunza jinsi mashirika katika jamii anuwai yatakavyoifanya kazi hii.

Kuhusu demografia za washiriki, hakuna matarajio ya chini zaidi kutoka kwenye ofisi yetu, lakini ikiwa hiki ni kipengele muhimu cha pendekezo lako, tafadhali hakikisha kuwa umebainisha jinsi utakavyokishughulikia na utoe sababu ya umuhimu wacho. Hili linaweza kuwa msingi wa majibu yako ya S#15, 19, na 21.

10. **Kutoka S#17 katika fomu ya ombi, unataja kuwa mashirika yanayopata ruzuku yanapaswa kupanga angalau kundi moja (1) la majadiliano. Je, unatarajia mashirika kupanga zaidi? Na ikiwa ndivyo, yanapaswa kuwa katika lugha tofauti, au linaweza kuwa kundi jingine kutoka lugha moja?**

Tunaelewa kwamba mashirika mengine yanatumia lugha zaidi ya moja, au kuwa washirika wengine wanaweza kuzungumza lugha zaidi ya mbili. Matakwa yanabainisha angalau kundi moja la majadiliano ana kwa ana na kutegemea na uwezo wa shirika tutafurahia zaidi ya lugha moja lakini si lazima. Tafadhali fahamu kwamba hii ni fursa

yenye ushindani na kuwa ikiwa shirika lako lina uwezo wa kukusanya maoni katika lugha zaidi ya moja hilo litafanya liwe na ushawishi.

11. **Kutoka S#22 katika fomu ya ombi, je, shirika letu litapokea maoni ya zamani baada ya kundi la majadiliano kuisha ili kuweza kushiriki matokeo na washiriki?** Mashirika yaliyoteuliwa yatakuwa na jukumu la kuandaa na kuwasilisha matokeo. S#22 linauliza shirika kuhusu matokeo ya makundi ya majadiliano ili Ofisi ya Wahamiaji iweze kujumuisha maoni katika mkakati wa ushirikishaji na rasilimali za lugha.

    Maombi yanapaswa kubainisha jinsi shirika linavyopanga kusimamia shughuli za makundi ya majadiliano na kukusanya matokeo. Pindi tu unaposimamia makundi ya majadiliano na kurejesha nyaraka kwenye Ofisi ya Wahamiaji, tutapitia wasilisho lako la nyaraka za mradi na kuwasiliana nawe ikiwa ufafanuzi zaidi unahitajika.

12. **Mradi huu unaangazia lugha. Je, ni mapendekezo gani yanayotolewa kuhusu mahusiano kati ya lugha na athari ya utamaduni na utambulisho wa utamaduni? Kwa mfano, Kihispania ni lugha moja lakini yenye tamaduni nyingi ambazo zinakutanisha tabaka na jinsia katika nchi zote (Mfano, njia tatu za kuwaamkia watu "tu," "vos," "usted".)**

    Fikra kuhusu lugha ndiyo maudhui haswa ambayo tungetarajia kujadiliwa kwenye makundi ya majadiliano. Ofisi ya Wahamiaji kwa sasa ina mtaalamu ambaye amekuwa akikutana na wanajamii katika lugha zadi ya 9 lakini sasa tunayahimiza mashirika kuongoza mchakato huu na kusimamia mazungumzo kuhusu lugha ambayo huenda yasianzishwe na serikali ya jiji ila jamii. Katika ombi, tulisisitiza umuhimu wa mwezeshaji na katika S#16, tunafanya maksudi tunapouliza jinsi mwezeshaji alivyojitayarisha kuongoza kundi la majadiliano na kukusanya maoni ya maandishi na ya kusemwa.